Jarida la Kiswahili Sanifu

Mwingilianomatini katika Riwaya za *Siku Njema* na *Utubora Mkulima*

Emmanuel Nthuka[1] Aidah Mutenyo[2]
[1]Chuo Kikuu cha Ohio, Marekani; ustadhemmanuel254@gmail.com
[2]Chuo Kikuu cha Kabale, Uganda; aidahmutenyo@gmail.com

IKISIRI

Kila msanii huwa na upekee wa kimtindo katika kuisuka kazi ya fasihi na vilevile wasanii tofauti aghalabu huandika kazi zao katika awamu tofauti za kihistoria na kiwakati. Licha ya haya, mwingiliano wa namna fulani huelekea kutokea kati ya kazi husika za kisanaa za wasanii. Hivyo basi, makala hii inatathmini mwingilianomatini kati ya riwaya ya *Utubora Mkulima* (Shaaban, 1966) na *Siku Njema* (Walibora, 1996) huku ikiongozwa na nadharia ya Mwingilianomatini iliyoasisiwa na Julia Kristeva (1980) na kuendelezwa na wataalamu kama vile Allen, Mikhail Bakhtin na Ferdinand De Saussure. Data za kazi hii zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya udurusu wa makala za kitaaluma maktabani. Uchambuzi wa data ulifanywa kupitia mbinu ya uchambuzi wa kimaudhui. Utafiti huu umebainisha kuwa kuna mwingiliano wa kisifa baina ya wahusika katika riwaya hizi mbili kama vile sifa ya upweke, bidii, uadilifu, uwerevu na utajiri. Aidha, kuna mwingiliano kimaudhui kuhusu kazi hizi mbili kama vile kazi, mapenzi na kifo. Utafiti huu utawasaidia wanachuoni katika kuelewa na kuangalia kazi za nyanja nyinginezo za kifasihi kimwingilianomatini.

KUHUSU MAKALA

Maneno Muhimu:
Mwingiliano matini, Maudhui Riwaya, Wahusika,

Historia ya Makala:
Tarehe ya Kutumwa:03 April 2024
Tarehe ya Kurekebishwa:14 Sept 2026
Tarehe ya Kukubalika:15 Sept 2026
Mtandaoni: 16 Oktoba 2026

*Mwandishi Mkuu. Simu: 220-224-9291; *Barua Pepe* ustadhemmanuel254@gmail.com
Mhariri: Frida Miruka, Chuo Kikuu cha Masinde Muliro, Kenya.
Nukuu: Nthuka, E. & Mutenyo, A. (2026). Mwingilianomatini katika Riwaya ya *Siku Njema* na *Utubora Mkulima*: 3(2), 130-139
© 2026
Creative Commons Attribution License (CC BY-NC-SA)

1.0 Utangulizi

Riwaya ni utanzu wa fasihi ambao unategemea zaidi ulimbwende wa vitushi na jinsi vinavyozuana na kusababishana; wahusika wakiwa nyenzo kuu (Njogu & Chimerah, 1999). Njogu na Chimerah (1999) wanaendelea kueleza zaidi kuwa riwaya ni tungo ndefu yenye kubuni inayoeleza hali fulani katika maisha ya binadamu kwa kutumia lugha nathari. Watt (1957) anasema kwamba kuibuka kwa riwaya kulitokana na ongezeko la tabaka la kati huko Uropa Magharibi. Mabadiliko makubwa ya kijamii na kiuchumi yalipelekea riwaya kuwa maarufu. Vilevile, maendeleo katika teknolojia ya uchapishaji yalifanya maandishi kupatikana kwa idadi kubwa ya wasomaji. Kwa mantiki hiyo, mabadiliko katika njia za usambazaji na viwango vya kusoma na kuandika yalileta vitabu na vipeperushi kwa watu waliotengwa na elimu, kama vile wanaume na wanawake wa tabaka la chini.

Hali hii iliwafanya waandishi wa kule Uropa kuwa mawakala huru katika soko la fasihi, wakitegemea mauzo maarufu kwa mafanikio na riziki, na pia wakionesha maadili na elimu ya tabaka la kati na la juu. Baadaye, riwaya za kisasa ziliibuka kutokana na waandishi wa wakati huo kama vile *Don Quixote* ya Miguel de Cervantes (sehemu ya kwanza iliyochapishwa mnamo 1605), na baadaye *Novelas Exemplares,* iliyochapishwa mnamo 1613. Don Quixote inachukuliwa kuwa mfano wa riwaya ya kisasa kwa sababu ilishiriki malengo mengi na riwaya za leo. Kitabu hiki kinajumuisha maoni ya kijamii na ukosoaji wa kifasihi.

Mulokozi (2017) anasema kwamba watunzi wa awali walitunga riwaya kwa kusukumwa na mabadiliko ya kijamii ya karne ya 16-18 huko Ulaya ambapo fani za jadi kama vile ngano, hekaya, tendi, visakale, sira, masimulizi ya wasafiri, insha na tafsiri zilichangia katika uandishi wa riwaya. Ni kutokana na mazingira ya kijamii ambapo riwaya za Kiswahili zilianza kuchipuka kama vile *Adili na Nduguze* (Shaaban, 1952), *Kusadikika* (Shaaban, 1951), *Lila na Fila* (*Kiimbila*, 1966) na nyinginezo. Njogu na Chimerah (2011) wanasema kwamba riwaya ya Kiswahili imeingia baada ya ukoloni wa kimagharibi lakini kifani na kimaudhui ina asili yake katika ngano za fasihi simulizi ya Kiswahili. Tungo za awali ziliweka msingi ambao uliigwa na kuendelezwa na tungo za baadaye kwa njia ya mwingiliano wa matini.

Mwingiliano matini sio swala geni katika fasihi ya Kiswahili. Nadharia ya Mwingilianomatini imepata kufasiriwa na kuhusishwa na wataalamu wengi kama vile Kristeva (1980), Abrams (1981), Bakhtin (1981), Syambo na Mazrui (1992) na Alfaro (1996). Kwa kuweka uzito katika kazi ya mwingiliano matini na ishara, De Saussure (2006) anakazia suala la matumizi ya ishara katika lugha. Kristeva (1980) pamoja na wataalamu wengine wa mwingilianomatini kama vile Barthes (2007) na Haberer (2007) wanaamini kuwa msomaji wa pekee ni yule mwandishi asomaye matini nyingine hali inayopelekea matini kujisoma yenyewe huku ikijiandika yenyewe.

2.0 Suala la Utafiti

Kazi za kifasihi huundwa kutokana na mifumo ya kanuni na tamaduni mbalimbali zilizowekwa na kazi tangulizi za kifasihi ambapo taswira za maisha ya kawaida na uhusiano wa kimaana huelekea kuunganishwa na kubadilishwa (Kristeva, 1977). Kristeva (Keshatajwa) anasisitiza kwamba watunzi hawabuni matini kutokana na fikra zao wenyewe bali hukusanya mawazo kutoka kwa matini ambazo zipo. Hivyo basi, matini ni mkusanyiko wa mawazo ya watu katika jamii kwa ujumla. Makala hii inadhihirisha kauli kwamba binadamu yeyote ulimwenguni aghalabu hutatizwa na masuala sawa. Aidha, waandishi wa kazi za fasihi huweza kulelewa katika mazingira yaliyo tofauti kimaeneo lakini wakaandika matukio yao katika kazi zao kwa njia zinazolandana.

Kwa hivyo, kazi za fasihi huingiliana kimaudhui na kifani licha ya kutungwa katika nyakati na mazingira tofauti na pia waandishi tofauti. Kila mwandishi huwa na upekee wake kimtindo katika kuisuka kazi ya fasihi (Syambo & Mazrui, 1992). Aidha, utafiti huu utapanua uwanja wa fasihi linganishi kwa kukuza suala la mwingilianomatini kwa kulinganisha riwaya za *Siku Njema* (Walibora, 1996) na *Utubora Mkulima* (Shaaban, 1966) katika kazi za fasihi.

3.0 Uhakiki wa Maandishi

Kwa mujibu wa Shitakwa (2018), kuna kazi za tanzu nyingine za fasihi andishi ya Kiswahili ambazo zimetumia nadharia ya mwingilianomatini kama vile: *Sitaki Iwe Siri* (Matundura, 2008) inayoingiliana na *Nataka Iwe Siri* (Kirumbi, 1974); *Usiku Utakapokwisha* (Msokile,1993) inayoingiliana kimaudhui na *Giza Limeingia* (Mbogo, 1980); na vilevile *Mashetani* (Hussein, 1971) inayoingiliana kimaudhui na *Kijiba cha Moyo* (Arege, 2009).

Njoroge (2007) alihakiki mwingilianomatini wa kimaudhui wa riwaya mbili za waandishi wawili, *Rosa Mistika* (Kezilahabi, 1971) na *Tata za Asumini* (Mohamed, 1990). Aidha, Njoroge (keshatajwa) alitalii vipengele anuwai katika mawanda ya kimwingilianomatini kama vile ploti, wahusika, mandhari na maudhui. Nadharia iliyoongoza utafiti wake ilikuwa mwingilianomatini. Alionesha pia namna riwaya hizi zinavyohitilafiana kwa kiasi tu katika kipengele cha ploti na wahusika.

Kwa upande mwingine, Bosire (2016) alichunguza mwingilianomatini katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (Gogol, 1836) inayoingiliana na riwaya ya *Mstahiki*

Meya (Arege, 2009). Mtafiti huyu alichunguza vipengele kama vile ploti, wahusika, mandhari na maudhui. Alidhihirisha kuwa kuna mwingiliano wa kifani na kimaudhui katika tamthilia hizi mbili alizohakiki. Aidha, Bosire (2016) alitambua kwamba waandishi waliokuwa kwenye mazingira tofauti na vipindi tofauti vya wakati wanaweza kuathiriwa na masuala sawa katika jamii wanamoishi na kuandika kazi zinazolandana kwa kiasi fulani.

Utafiti kuhusu mwingilianomatini katika riwaya ulifanywa pia na Wamitila (2003a) aliyelinganisha riwaya mbili za *Nagona* na *Mzingile* za Euphrase Kezilahabi, na *Pedro Paroma* ya Juan (1995). Hapa, Wamitila (2003a) alihoji kuwa uhusiano uliopo baina ya hawa watunzi wawili ni wa kimwingilianomatini au wa usemezano wa kisanaa. Aliongeza kwa kusema kuwa Kezilahabi mwenyewe anakiri kuisoma *Pedro Paroma* kabla ya kuziandika hizi riwaya zake. Kwa hivyo, taathira ya Juan Ruflo inadhihirika katika riwaya za Kezilahabi. Katika riwaya zote tatu, kuna taswira na mbinu nyingine ambazo zimetumika ili kuunganisha vipengele anuwai katika mseto mmoja imara. Pia, alionyesha mfanano wa kimaudhui na kifani baina ya riwaya za hawa watunzi wawili.

Wanyela (2007) alishughulikia mwingilianomatini katika tamthilia tatu za Kiswahili hasa *Kilio cha Haki* (Mazrui, 1981), *Mama Ee* (Mwachofi, 1987) na *Amezidi* (Mohamed, 1995) na kuhitimisha kuwa tamthilia hizo ziliingiliana kimaudhui na kiuhusika.

4.0 Matokeo na mjadala

Makala hii ilipata data kutoka riwaya mbili ambazo waandishi wameandika katika vipindi tofauti na nchi tofauti lakini visa na maudhui yanaibukia kuingiliana kwa kuhusisha mawazo na mihimili ya nadharia ya mwingiliano matini. Hivyo basi, mawazo na mihimili ya mwingilianomatini inadhihirika katika *Siku Njema* na *Utubora Mkulima* kwa kutumia sifa za wahusika.

4.1 Mwingilianomatini kati ya *Siku Njema* na *Utubora Mkulima*

Kuna aina mbalimbali za mwingilianomatini katika kazi hizi mbili; mwingiliano wa wahusika, kimaudhui na kifani

4.1.1 Mwingilianomatini wa wahusika katika *Siku Njema* na *Utubora Mkulima*

Wahusika ni viumbe hadithini ambavyo hutumiwa na mtunzi kujenga jumuiya au jamii inayojitokeza katika kazi ya kifasihi. Wamitila (2003b) na kina Waititu na Ipara (2013) wanasema kuwa wahusika ni viumbe wanaopatikana katika kazi ya kifasihi na ambao wanafanana na binadamu kwa kiasi fulani. Njogu na Wafula (2013) wanasema kwamba wasifu wa wahusika unategemea mkabala uliopo. Kazi zinazoegemezwa katika mitazamo ya kihalisia zinawasawiri wahusika kwa namna inayokaribiana sana na binadamu katika ulimwengu wa kawaida. Ulimwengu ambao jamii inakabiliana na matatizo yanayohusiana na jamii inayopanuka (Njogu & Wafula, 2013).

Kwa mujibu wa Madumulla (2009), mhusika hudhukuriwa kama picha inayochorwa na fasihi na kuwa chanzo cha vitu vyote vipya zikiwemo dhamira na mada katika fasihi. Sehemu inayofuata inajadili mwingiliano wa sifa za wahusika katika riwaya hizi mbili.

4.1.2 Sifa ya Upweke

Riwaya za *Siku Njema* na pia *Utubora Mkulima* zinaonesha kuingiliana katika wahusika na uhusika kwa kiwango kikubwa. Katika riwaya ya *Siku Njema*, kuna wahusika ambao wanaafikiana na wahusika katika *Utubora Mkulima* katika hulka zao. Sifa kuu inayoonekana katika wahusika hawa wawili yaani Mzee Kazikwisha katika *Siku Njema* na Bimkubwa katika *Utubora Mkulima* ni upweke. Wanaishi katika sehemu ambazo zimetengwa. Wamejitenga na wanajamii na hivyo kuishi katika maisha ya kipweke sana. Mathalan, katika riwaya ya *Siku Njema*, kuna mhusika Kazikwisha ambaye anaishi peke yake katika lindi la upweke; hana mtoto yeyote na asili yake haijulikani. Tazama nukuu hili.

> "...Mzee Kazikwisha alikataa kuchangamana na watu. Watu nao walimwona kama mkia wa mbuzi na apizo kubwa. Watu walimuambaa kama mkoma. Walimwogopa kama mgonjwa wa maradhi mabaya ya kuambukiza…. Muradi mzee Kazikwisha aliishi kama kisiwa katikati ya bahari." (*Siku Njema*, uk. 117).

Mzee Kazikwisha anaishi Makutano ya Ngozi ambako anaishi peke yake kwa miaka mingi sana. Watu wanamwona kama mgumba kwa kukosa mwana. Anapokutana na mhusika mkuu Msanifu Kombo, anavutika naye na kumwomba aende kwake.

Sehemu moja ya maisha ambayo ni muhimu sana kwa upweke ni ya familia na uhusiano. Kanuni ya maisha ni "maisha yaliyounganishwa" ambayo inasisitiza jukumu muhimu linalochezwa na kijamii na mahusiano katika kutathmini matokeo ya maisha (Goodenow na wenzake, 2016; Hsieh & Liu, 2021; Perales & Campbell, 2020). Mara nyingi ni kwa njia ya mahusiano ya karibu na mwingiliano baina ya watu ambapo athari hasi ama chanya za kitamaduni wa kijamii husikika zaidi. Kwa mfano, Mzee Kazikwisha alitengwa na jamii yake kiasi kwamba alifikirika kuwa na maradhi ya kuambukiza.

Utafiti huu ulibaini kwamba mhusika Kazikwisha katika riwaya ya *Siku Njema* anaingiliana kisifa na mhusika mkuu Bimkubwa katika riwaya ya *Utubora Mkulima*. Bimkubwa amejifungia ndani kwa majonzi na upweke. Anaachiwa mjukuu ambaye vilevile anakufia vitani na likarudi jina tu. Toka hapo

anajifungia ndani na kukataa kufarijiwa. Watu wanaoonana naye ni wanawake wawili tu ambao ni watumishi wake wa ndani. Haya yanadhihirika katika dondoo hili;

> "Bimkubwa alikaa Busutamu tangu kuolewa. Alikuwa na watoto wawili: mwana na binti, lakini mwana alitangulia kufa akabaki na binti aliyeishi mpaka akaolewa. Vita vilipotokea kijana huyu aliungana na majeshi akaenda kupigana. Kwa bahati mbaya, alipatwa na mauti ya ushujaa likarudi kwao jina tu. Tangu wakati ule bibi yake alijifungia ndani akakataa kufarijiwa. Alikaa peke yake kulia na kuomboleza juu ya msiba wake." (*Utubora Mkulima,* Uk. 43-44).

Radhia anasema kuwa Bimkubwa aliishi maisha ya kipweke:

> "Ana fedha nyingi, na kama ataka kukaa maisha ya upweke, mimi nafikiri ni kwa sababu anapenda upweke." (*Utubora Mkulima*, Uk. 27)

Upweke huathiriwa na mambo kadhaa ikiwa ni pamoja na umri, hali ya ndoa, mitandao ya kijamii na ushiriki, hali ya upungufu wa utendaji kazi na afya ya akili (Aartsen & Jylha, 2011; Bosma na wenzake, 2015; Cacioppo na wenzake, 2010; Fokkema na wenzake, 2012; Hansen & Slagsvold, 2015). Vile vile upweke huweza kutokea kwa mtu yeyote iwe mdogo kwa umri ama mkubwa. Katika *Siku Njema na Utubora,* wazee wawili wameathirika hasa kutokana na kupoteza jamaa wa karibu na kukosa matumaini ya kuona jamaa waliotengama nao.

Mzee Kazikwisha anaishi bila mtoto wake wa kipekee naye Bimkubwa mwanawe anakufia Burma vitani. Hali hii inawazidishia upweke. Mzee Kazikwisha na Bimkubwa wote wana sifa ya kukaa kimya (Upweke). Hawazungumzi na majirani wao wala mtu yeyote hadi wanapokutana na wahusika wakuu. Bimkubwa ana wafanyikazi wawili tu hao ndio anazungumza nao naye Kazikwisha hasemi na yeyote hadi Msanifu Kombo anapotokea na kusema naye kama tunavyoona katika dondoo hili:

> "Mzee Kazikwisha alikataa kuchangamana na watu. Watu nao walimwona kama mkia wa mbuzi na apizo kubwa. Aliishi kwa ukiwa mkubwa. Watu walimuambaa kama mkoma. Walimuogopa kama mgonjwa wa maradhi mabaya ya kuambukiza." (*Siku Njema,* Uk 117).

Njogu na Wafula (2013) kwa kurejelea wataalamu mbalimbali wameeleza kwamba kazi nyingi za kifasihi huelezea maisha ya binadamu jinsi yalivyo na mazingira anapopatika mwanadamu. Wanaendelea kusema kwamba matendo ya wahusika yanachochewa na mambo kama vile hali ya kisaikolojia inayowazunguka. Hivyo basi, kazi ya mwandishi ni kuonesha namna hali ilivyo. Kwa vile kazi ya fasihi ni kuwa kioo cha jamii, mwandishi anastahili kuonesha picha namna ilivyo bila kuitilia chuku.

Kwa mfano, Bimkubwa alipoondokewa na wanawe na mjukuu wake anaishi kwa kuwaambaa watu hataki kusemezana na watu anajifungia ndani kwa miaka mingi. Anaishi maisha ya kutotaka kutangamana na watu. Anachukia kila kitu. Haoni maana ya kuishi ama kubaki katika hali aliyomo. Ili kumtoa katika hali ya upweke na kumrudisha kutangamana na jamii inastahili ustadi na uhodari wa hali ya juu sana. Ndiyo maana Utubora anasema;

> "Namsikitikia Bimkubwa huyu siku zote, hata kupita karibu na nyumba hii hunihuzunisha kabisa." (*Utubora Mkulima,* Uk. 27)

> "Lakini yeye ni mzee sana na sisi sote hatukuumbwa namna moja. Naamini kuwa yeye hatoki nje hata kidogo, hata hendi katika kiunga chake, zamani alizoea kutoka nje…" (*Utubora Mkulima*, Uk. 28)

Hii ina maana kwamba Bimkubwa alitoka na kutangamana na watu wakati alikua katika furaha na jamii yake na maisha yalikua kama ya wengine lakini baada ya kufiwa na mumewe na watoto wake hali ilibadilika.

4.1.3 Sifa ya Bidii

Wahusika wakuu, Msanifu Kombo na Utubora wana sifa ya bidii. Wanatia bidii sana katika maisha hasa kwenye kazi za mkono au vibarua. Katika riwaya ya *Siku Njema*, Msanifu Kombo anamsaidia rafiki ya mjomba wake, Athman katika kazi za useremela. Anasema;

> "Hatimaye Athman Ali, seremala mmoja wa Tanga rafikiye mjomba Kitwana, aliniajiri kama msaidizi wake. Niliondokea kuwa stadi sana katika kupiga vyombo msasa, na kuvirandia." (*Siku Njema*, Uk. 27)

Hali ya Msanifu Kombo ya kuwa yatima na kupitia mateso mengi yalimfanya awe kijana mwenye bidii kwa kila jambo. Vumulia (rafiki wa Msanifu Kombo) alikuwa ameshamtahadharisha kuwa makini na mkaza mjomba wake na Bi. Rahma. Tangu atambue kwamba wawili hawa walikua tayari kuangamiza maisha yake, alifanya kila liwezekanalo ili atoke Tanga. Wamitila (2008) anasema kwamba ili fasihi ishahibikiwe ni vyema ihusishwe na mwigo wa ukweli wa maisha ya kijamii.

Hivyo, Kongowea anatimiza lengo lake na kuanza mwendo wake wa kuenda kumtafuta babake. Kongowea anapofika Mombasa, anakutana na Rashid na kuishi naye lakini Rashid anaishia kufa. Kongowea anabaki Mombasa maanake alikwenda kumtafuta Bakari Makame ambaye ni mjomba wake lakini anamkosa. Anaishia kuwa mchoraji ili kujipatia riziki. Anasema:

> "Sikuwa na mtaji wowote wa kuanzia uchoraji. Zawadi na Amina wakanifadhilia fedha za kununulia rangi, brashi, karatasi na ala zilizohitajika. Aghalabu nilichora nyuso za watu na kuwatoa namna walivyo haswa." (*Siku Njema*, Uk, 92)

Ni kupitia hela hizi ambapo Msanifu Kombo anatumia kama nauli ya safari yake ya bara kwenda kumtafuta babake. Mfano mwingine ni pale Msanifu Kombo anapofika Makutano ya Ngozi anakutana na Bi Mercy MacDonald ambaye anampa kazi:

> "Bi. Mercy akanipa kazi, lakini nyepesi si ya sulubu. Kazi yangu ikawa kufagia majani kiamboni, kufyeka nyasi, kupalilia na kunyunyuzia maua kwenye bustani na kulengeta ua. Mshahara wangu ulikuwa shilingi mia moja ishirini kwa mwezi…" (*Siku Njema,* Uk. 111)

Msanifu Kombo anafanya kazi kwa Bi. Mercy hadi anapokutana na Mzee Kazikwisha na kupata urithi wake. Mwandishi Ken Walibora anadhihirisha uhalisia wa changamoto mbalimbali ambazo mtoto wa Kiafrika hupitia hasa kijana ambaye hana matumaini ya kupata urithi wowote kutoka ujombani. Kwa vijana ambao hawana hekima huishia kufanya maovu kama mhusika Sulemani. Ila vijana ambao walilelewa kwa maadili kama Msanifu Kombo ilikua ni dhahiri kutumia maadili kufanikisha matakwa yake.

Kwa upande mwingine katika riwaya ya *Utubora MKulima*, Utubora anafanya kazi kama karani katika ofisi ya serikali anaonekana mwadilifu na mwenye bidii. Tunaambiwa kuwa:

> "Kwa kushika majira alikuwa kama saa; na mahudhurio yake mema katika kazi hayakuwezekana kushindwa na watumishi wengine. Kila siku alikuwa mtu wa kwanza kuhudhuria kazini, wakati wenziwe walipokuwa wamechelewa; na wa mwisho kuondoka kazini, wakati wengine walipotangulia kwenda zao. Laiti watumishi wote wangekuwa kama Utubora, ugumu katika mioyo ya matajiri ungalilainika." (*Utubora Mkulima,* Uk 1)

Utubora anaonekana kuwa mwenye bidii kazini mpaka kufikia upeo wa kusifika kazini. Anapotaka kuacha kazi bwana Ahmed anasikia vibaya. Mke wa Liwali anapotafuta mtu wa kumfanyia kazi mwenye bidii anapendekezewa na Bihaya kuwa Utubora ni mtu bora. Imamu anamwajiri Utubora kumtolea gugu lake ambalo limekuwa kubwa sana. Utubora bado anamlimia Bimkubwa gugu lake ambalo limemea hadi mlangoni:

> "Alichagua kuanza kazi yake katika upande wa mbele ya nyumba. Alifikiri kuwa labda Bimkubwa akiona kazi inaendelea atapendezwa au pengine hata audhike sana…" (*Utubora Mkulima,* Uk. 45)

Mfano wa dondoo hili unadhihirisha mwingiliano matini ya uchapa kazi kwenye riwaya ya *Siku njema* na ile ya *Utubora.* Katika matokeo ya utafiti huu, inaonyesha dhahiri kwamba katika jamii hutokea shughuli za kijamii ambazo zinataka kukamilishwa. Hivyo basi, jamii vilevile iko makini sana kuelekeza kinachofanywa. Katika *Utubora Mkulima,* mwandishi anachukua muda akizungumzia shughuli kwa muda mrefu. Shughuli hii inajitokeza kwa maongezi ambayo yanamsawiri Utubora kama mhusika wa kutegemewa kazini na ndiyo maana anapendekezwa na Bihaya.

4.1.3 Sifa ya Uadilifu

Wahusika wakuu katika riwaya hizi wanaonekana kuwa wenye uadilifu sana na kujidhibiti kwa hali ya juu. Ni watu ambao wanaepukana na mambo mengi kutokana na uadilifu wao. Katika riwaya ya *Siku Njema*, Msanifu Kombo anaonekana kuepukana na ufuska na majaribu. Anapofika Mombasa, anakutana na Amina wakiwa kwenye safari ya meli. Amina anampeleka kwake na kumpikia wali wa pukute. Kisha anaoga mbele yake na anapomaliza anamwambia:

> "Ndoo tulale"

> "Isitoshe wewe mwenyewe ni kijana mzuri sana. Hakuna cha kutuzuia..." (*Siku Njema.* Uk .58)

Msanifu Kombo anakataa ombi lake na kumjibu:

> "Kunalo la kutuzuia, Litakalotuzuia ni heshima. Suala la sisi kulala pamoja halina mashiko murua. Nakuheshimu sana na kujiheshimu mwenyewe… Tusidanganyike. Afadhali kutahadhari kabla ya hatari." (*Siku Njema*, Uk. 58 - 59)

Msanifu Kombo anaonesha tena uadilifu wake anapomkataa Zawadi ambaye alikuwa mpenzi wa rafiki yake Rashid ambaye alikufa. Zawadi anakiri kusalitika kimapenzi na Kongowea. Lakini Kongowea anamwambia huko ni kumkosea heshima rafiki yake marehemu?

> "Wewe. Nakupenda sana. Nataka unioe." (*Siku Njema,* Uk. 97)

> "Mimi sikufai wewe Zawadi… Tena nilimpenda sana marehemu Rashid. Sitaki iwe habari ya paka akitoka panya hutawala…. Na maana matumaini yangu ya mustakabali hayalingani na yako. Tunayo matumaini tofauti..." (*Siku Njema*, Uk 97 – 98)

Miaka mingi baadaye, Zawadi anatazama nyuma na kuona kweli Kongowea alikuwa mwadilifu. Anamwandikia barua na kumshukuru na kumjulia hali manake kipindi hiki amehamia bara. Hali hii imeelezwa na mwandishi wa *Siku Njema* kuonesha namna dunia imebadilika kulingana na mahitaji ya mtu binafsi. Kwa uadilifu ambao Msanifu Kombo alionao anamuelezea bila kumdhihaki Zawadi jinsi ni vigumu kumuoa. Kuanzia kwa umri, ndoto na mahitaji ambayo kila mtu yuko nayo.

Mfano mwingine wa kuonesha uadilifu wa Kongowea kimapenzi ni pale anapokataa Alice ambaye anakuja chumbani kwake na kumtaka kimapenzi. Kongowea anaepuka mtego huu kwa mara nyingine na kuthibitisha uadilifu wake.

> "Alice humu wataka nini sasa hivi?..." (*Siku Njema,* Uk. 115)

> "Basi nenda kalale chumbani mwako…" (*Siku Njema,* Uk .115)

> "Punde si punde, Alice aliyekuwa kasimama karibu na mlango alikuja kuketi nchani mwa kitanda changu na kujaribu kunipapasa. Nikanyanyuka pole pole na kuondoka chumbani kama ambaye naenda msalani. Nikaenda mpaka kwenye banda la John, mchungaji wa ng'ombe wa Bi. Mercy na kuomba mahali pa kulala. Tangu hapo nilienda kuishi na mchungaji hata baada ya Bi. Mercy kurejelea kutoka safarini…" (*Siku Njema,* Uk. 115 – 116.)

Katika riwaya hii, Kongowea anadhihirisha sifa ya uadilifu kwa kutotetereka na kunaswa na mtego wa mapenzi ya kiholela. Katika riwaya ya *Utubora Mkulima*, Utubora alikuwa mwadilifu kazini sana. Uadilifu wake unatokana na kufika kazini mapema na kuwa wa mwisho kuondoka na pia kufanya kazi yake vizuri:

> "Utubora alistahili sana ijara kubwa kama hiyo kwa sababu ya sifa alizokuwa nazo. Alikuwa mtu imara mbele ya telezi nyingi, kama vile hiana na mengine; mvumilivu mbele ya majaribu magumu, kama rushwa hodari mbele ya mashaka mazito, mfano wa kushika amana au dhima kubwa; mwaminifu kama mchana na msiri kama usiku. Kila siku alikuwa wa kwanza kuhudhuria kazini, wakati wenziwe walipokuwa wamechelewa; na wa mwisho kuondoka kazini, wakati wengine walipotangulia kwenda zao." (*Utubora Mkulima,* Uk. 1)

Ahmed anaposikia Utubora anataka kutoka kazini na kuiacha, anaumwa sana kwa sababu anajua bidii na uadilifu wake kazini. Anampa muda wa kubadilisha wazo lake ila Utubora hatereregi katika mtazamo wake.

Wahusika wakuu katika riwaya hizi mbili hasa Msanifu Kombo na Utubora wanakataa uchumba licha ya kuwa wanawake waliowapenda walikuwa wamejitolea kwa hali na mali. Utubora anamkataa Sheha ambaye alikuwa mpenzi wake wa zamani kisha akaolewa, Utubora alipoenda vitani Burma. Anarudi baada ya ndoa yake kuvunjika na kumtaka Utubora kimapenzi lakini anamkataa.

4.1.4 Sifa ya Uwerevu

Licha ya kuwa wahusika wakuu walikuwa werevu sana shuleni hawamalizi masomo yao kwa sababu ya kukosa karo baada ya wazazi wao kuaga. Katika riwaya ya *Siku Njema,* Msanifu Kombo anaacha shule baada ya kufaulu darasa la saba na kuwa kati ya wanafunzi bora waliofaulu. Kwa kipindi hiki, mamake ambaye ni Zainab Makame alikuwa amekufa na inambidi kwenda kuishi na Mjomba wake Kitwana ambaye hakuwa na hela za kutosha za kumsomesha:

> "…ndoto ya kusoma hadi chuo kikuu nihitimu ama udaktari au urubani halikuweza kutimia kamwe. Mjomba Kitwana alikuwa na nia ya kunilipia karo lakini maradhi ya mkono yalimaliza pesa zake zote katika kujaribu kuyaganga." (*Siku Njema,* Uk. 27)

Masomo ya Kongowea yanamalizikia hapo kwa kukosa karo ya shule licha ya kuwa mwerevu sana masomoni. Vilevile, katika riwaya ya *Utubora Mkulima*, Utubora alisoma sana hadi chuo kikuu na alikuwa bingwa masomoni lakini anaacha shule kwa kukosa karo. Makuu anamweleza Radhia kuwa Utubora aliacha shule baada ya ukosefu wa karo:

> "Nakumbuka kuwa ilimpasa kuondoka chuoni. Hakungoja kuhitimu kwa sababu baba yake alikuwa amefilisika alipokufa."

Tunaona kuwa kuna mwingiliano kati ya matukio ya wahusika hawa wawili na ukosefu wao wa karo baada ya wazazi wao kufilisika na kufa. Mamake Kongowea, Zainab anafilisika na kufa akiwa maskini kutokana na ugonjwa aliokuwa nao ambao ulimaliza mali yake. Kifo cha mzazi huleta simango katika maisha ya mtoto. Maisha ya mtoto yanaingia katika

hali taharuki hasa pale ambapo anakosa uhakika wa kifedha. Iwe ni wazazi ambao wametengana au talaka ama kifo mara nyingi anayeathirika ni mtoto.

4.1.5 Sifa ya Utajiri

Wahusika wote wawili Kazikwisha na Bimkubwa kutoka kwa riwaya zote mbili ni watu walio na mali nyingi sana ila mali yao haina faida kwao. Kazikwisha ameishi kwa miaka mingi sana peke yake na mali yake kukosa mwangalizi hadi anapotokea Msanifu Kombo na kuirithi baada ya kifo chake. Vilevile, Bimkubwa ana mashamba na fedha nyingi sana lakini mali hii yote inakosa mwangalizi hadi anapotokea Utubora na kuirithi baada ya kifo chake. Msanifu Kombo anasema hivi katika riwaya ya *Siku Njema:*

> "Baada ya kwenda kidogo nikaona kasri lake. Yasemekana alinunua shamba hilo na kasri hilo wakati wa serikali ya Kenya ilipoanzisha sera ya kuwapa Waafrika ardhi iliyotengewa wazungu enzi ya istiimari. Tulipita dimbwi la kuogelea lilojengwa na mzungu aliyemiliki shamba hilo…." (*Siku Njema,* Uk. 123)

Mzee Kazikwisha anapoaga dunia anamwachia mali yake Msanifu Kombo ambaye ni mwana wake. Ni wazi kuwa mhusika huyu alikuwa na mali nyingi:

> "Kulingana na wosia huo mimi nilikuwa mrithi wa raslimali aliyoihalifu Bwana Juma Mukosi, babangu mzazi. Thamani ya raslimali yote, kutia ndani pandakizi lake la shamba, ilikuwa shilingi yapata milioni nne unusu. Huo ulikuwa utajiri ulioniangukia ghafla kama matone ya mvua katika anga lisilokuwa na wingu…" (*Siku Njema,* Uk. 135)

Bimkubwa katika *Utubora Mkulima* pia alikuwa tajiri kupindukia. Alikuwa na fedha nyingi na shamba pia. Sifa hii tunaiona pia kwa Kazikwisha ambaye alikuwa na pesa lakini hakuzifurahikia:

> "Kwa nini wahuzunika? Hayumo katika dhiki ya kusikitikiwa. Ana fedha nyingi…" (*Utubora Mkulima*, Uk. 27)

Bimkubwa pia anapokufa, anamrithisha Utubora mali yake yote?

> "Bimkubwa alifariki dunia. Baada ya mwezi kupita ilitokea kuwa kwa wasia wa Bimkubwa, miliki yake yote ililazimu kwenda kwa Utubora. Utubora alilala maskini akaamka tajiri mkubwa" (*Utubora Mkulima*, Uk. 91)

Wahusika hawa wakuu wanarithi mali ambayo inawafanya kulala maskini na kuamka wakiwa matajiri. Kongowea anarithi mali ya mzee Kazikwisha ambaye alimiliki mashamba makubwa sana. Kazikwisha ni babake Kongowea na hivyo anamrithisha mwanawe mali.

Utubora naye anarithi mali ya Bimkubwa ambaye alikuwa rafiki mkubwa wake. Bimkubwa anapokufa anaacha wosia ambao unaonyesha kuwa Utubora ndiye mrithi wa mali ile.

Urithishaji mali na uandishi wa wosia ni jambo linatendeka katika baadhi ya jamii zetu. Hii inahusiana mara nyingine na maadili ya mali, na uhusiano kuathiriwa na utu wema. Ni watu wachache sana katika jamii zetu hufanya urafiki na kuwa karibu na wale tunaochukulia kuwa ni matajiri katika jamii zetu. Ikitokea kwa bahati nzuri kama vile Msanifu Kombo alijiweka karibu na Juma Mkosi na kumpa muda kama vile Utubora na Bimkubwa basi wao ndio hufaidika.

4.2 Mwingiliano matini wa Kimaudhui katika Siku Njema na Utubora Mkulima

Kimsingi kazi ya kifasihi ya kimwingilianomatini huwa na uwezo wa kuhusiana, kuingiliana na kurejeleana na kazi nyingine za kifasihi kwa njia tofautitofauti ikiwepo kimaudhui. Maudhui ni jumla ya yaliyomo katika katika kazi ya sanaa. Ni ujumbe ambao mtunzi wa kazi ya fasihi alidhamiria kuwasilisha kwa hadhira yake. Kulingana na TUKI (2004), maudhui ni jumla ya mawazo yote yanayozungumzwa katika matini. Kwa mujibu wa *Kamusi Pevu ya Kiswahili* (Kenya Literature Bureau [KLB], 2016), maudhui ni mawazo yanayopatikana kwenye kazi yeyote ile ya kisanaa. Katika riwaya za *Siku Njema* na *Utubora Mkulima*, waandishi wanazungumzia maudhui ambayo yanaonekana kufanana na kuingiliana.

4.2.1 Mwingiliano wa Maudhui ya Kazi

Kwa mujibu wa *Kamusi Pevu ya Kiswahili* (KLB, 2016) ni utendaji unaotumia nguvu ya akili au ya mwili ili kufikia lengo fulani. Katika riwaya hizi mbili, tunakutana na wahusika wanaofanya kazi mbalimbali. Wahusika wakuu Utubora na Msanifu Kombo wanaonekana kuendeleza maudhui ya kazi kama vile ukulima. Msanifu Kombo anapopata shamba la babake Mzee Kazikwisha analima:

> "Tangu nilipoupata ukwasi na upasi wa ghafla, nimejizatiti kufagia misitu na kunadhifisha shamba langu linifae kwa kilimo chenye tija." (*Siku Njema,* Uk, 136)

Naye Utubora anaacha kazi yake ili awe mkulima. Anajiita Mkulima wa Makataa:

> "Nitakwenda kujenga nyumba nzuri Mrima pahali ambapo mama yangu alizaliwa, na kazi yangu itakuwa ukulima."

> "Hivi sasa sijui mengi lakini naweza kulima, kukata miti msituni na kuichoma mahali ilipokatwa. Naweza pia kupiga matuta nikapanda mboga." (*Utubora Mkulima,* Uk.14)

Kwa kurejelea dondoo zilizopo hapo juu tunaona ya kwamba ukulima ni kitu muhimu sana. Katika jamii nyingi tunaona kwamba Inawezekana kuwa tajiri kwa kilimo, lakini si rahisi na inahitaji juhudi kubwa, kujitolea, na ujuzi wa biashara. Waandishi wote wanatujengea taswira kwamba ukulima si kazi mbovu. Mtu yeyote ambaye anamiliki ardhi kubwa basi ana fursa za kuwa na kipato kutoka kwa mavuno ya shambani kuliko yule hana kwani jembe huwa halidanganyi.

4.2.2 Mwingiliano wa Maudhui ya Mapenzi

Kamusi Pevu ya Kiswahili (KLB, 2016) inaeleza mapenzi kama hisia nzito ya moyoni ambayo humfanya mtu avutiwe au athamini mtu, kitu au jambo fulani. Katika riwaya zote mbili tunaona watu waliosalitika kimapenzi na wahusika wakuu ila wahusika hawa wakawakataa. Katika riwaya ya *Siku Njema*, Msanifu Kombo anamkataa Zawadi ambaye anampenda sana.

> "Wewe. Nakupenda sana. Nataka unioe." (Uk 97)

Msanifu Kombo akajibu;

> "Mimi sikufai wewe Zawadi… Tena nilimpenda sana marehemu Rashid. Sitaki iwe habari ya paka akitoka panya hutawala…Na maana matumaini yangu ya mustakabali hayalingani na yako. Tunayo matumaini tofauti..." (*Siku Njema,* Uk 97 – 98)

Katika riwaya ya *Utubora mkulima*, Utubora anamkataa Sheha ambaye alikuwa mpenzi wake wa zamani ila sasa hawapendani tena. Sheha anamwambia;

> "Utubora fahamu kuwa nakupenda. Najua kwamba nilikuwa mjinga lakini nimeadhibiwa na nimetubu. Kama humpendi mtu yeyote mwingine tafadhali turudi katika mapenzi yetu sijabadilika bado. Nimekuwa bora kuliko nilivyokuwa zamani, kwa sababu nimejifunza kujua thamani ya mapenzi ya mtu mwema." (*Utubora Mkulima,* Uk 75– 76)

Utubora alieleza polepole:

> "Lakini mabadiliko ninayo mimi sasa. Nilipenda mwanamke aliyekuwa haishi kamwe duniani bali vitendo vyake vilifunua macho yangu kuona nilivyohadaika. Hatuwezi kurudi katika mapenzi, itakuwa haiwezekani." (*Utubora Mkulima, Uk 76*)

Kulingana na dondoo hili, tunaona kuwa mapenzi yanayoanzishwa na wanawake kwa wahusika wa kiume wanaishia kukataliwa. Hii ni kutokana na uadilifu wa wahusika hawa na pia kutotaka kuvunja heshima yao. Katika tamaduni za Kiafrika ni vigumu sana mtoto wa kike kupendekeza hisia zake za mapenzi kwa mvulana. Inapotokea inaonekana kwamba msichana hana adabu na asipochunga anaweza kuchukuliwa kuwa kahaba ama mjuaji. Waandishi wametumia dhana hiyo ili kuingiza uafrika katika kazi zao na kuleta mvuto wa usomaji wa fasihi. Upande mwingine wa suala la mapenzi tunaona mapenzi yanayoanzishwa na wanaume nayo yanaishia kwa ndoa.

Ndalu na Babusa (2013), *Katika Kamusi Teule ya Kiswahili* wanaeleza ndoa kama uamuzi wa watu kukubali kirasmi kuishi pamoja kama mke na mume. Katika *Siku Njema*, Msanifu Kombo alimwoa Vumilia Binti Abdala ambaye alikuwa rafiki yake wa utotoni. Anasema;

> "Hakuna kitu cha kudumu ila mabadiliko yenyewe. Hiyo ndiyo ajabu yangu ya maisha. Mathalan Vumilia Binti Abdalla, rafiki yangu wa utotoni alihitimu elimu katika chuo kikuu. Sasa anafanya kazi ya ualimu na ni mke wangu." (*Siku Njema,* Uk 135)

Utubora naye anaishia kuoa Radhia ambaye alikuwa mpenzi wa Makuu rafikiye wa zamani lakini wakakosana. Utubora anasema;

> "Radhia nakupenda hadi sasa?"

> "Mapenzi yetu hayakubadilika karibuni tutaoana." "Siku ya pili palifanywa arusi ya Utubora na Radhia." (*Utubora Mkulima,* Uk. 91)

Mara nyingi huwa inaaminika kwamba ukioa rafiki yako basi ndoa itadumu. Mungu alimuumba binadamu na kuweka utaratibu wa kuwepo mahusiano kati ya mwanamke na mwaname ili uzao uendelee. Mapenzi yana jukumu muhimu katika ustawi wetu wa kihisia, ukuaji wa kibinafsi, na muunganisho wa kijamii. Kwa kutambua na kuthamini wingi wa upendo na mapenzi katika aina zake mbalimbali, watu binafsi husitawisha uelewaji wa kina zaidi wa magumu yaliyomo katika mahusiano ya kibinadamu na kuboresha maisha yao kwa ujumla.

4.2.3 Mwingiliano wa Maudhui ya Kifo

Kamusi Pevu ya Kiswahili (KLB, 2016) inaeleza kifo kama hali au tendo la kufikia mwisho wa uhai au kutokwa na uhai. Wazazi wa kiume wa wahusika wakuu wanakufa. Katika riwaya ya *Utubora*

Mkulima, hatujaelezwa zaidi kuhusu mama yake Utubora ila tumeelezwa kuhusu babake ambaye alikufa akiwa maskini. Katika riwaya ya *Siku Njema*, Kazikwisha anaaga dunia baada ya kukutana na mwanawe Msanifu Kombo:

> "Nilipofika nyumbani kwa Mzee Kazikwisha nikabisha, sikujibiwa…. Nikaingia chumbani mwa Mzee Kazikwisha…. Moyo waangu ulipasuka kwa yale… Mzee Kazikwisha alikuwa maiti. Babangu alikuwa tayari marehemu." (*Siku Njema,* Uk 134)

Utubora naye pia tunaelezwa katika riwaya ya *Utubora Mkulima* kuwa babake alikufa akiwa chuoni, jambo ambalo lilimpelekea yeye kutomaliza shule kwa ukosefu wa karo?

> "Nakumbuka kuwa ilimpasa kuondoka chuoni. Hakungoja kuhitimu kwa sababu baba yake aliendelea alipokufa alikuwa amefilisika au maskini…" (*Utubora Mkulima,* Uk. 32)

5.0 Hitimisho

Makala hii ilishuhulikia mwingilianomatini kati ya riwaya mbili ambazo ni *Siku Njema* na *Utubora*. Data za makala hii zimedhibitisha kwamba licha ya kuwa riwaya ya *Siku Njema* (1996) na *Utubora Mkulima* (1966) ziliandikwa katika mazingira na vipindi tofauti, usemazano katika riwaya hizi umesukwa kwa kiwango cha kukubaliana kwamba maisha ya binadamu ni mzunguko. Kinachomkera ama kumpendeza binadamu katika jamii moja ndivyo inavyotokea katika jamii nyingine. Hili limejitokeza kwa kutumia wahusika kuwasawiri kama wenye upweke licha ya kuwa na mali. Upweke unajitokeza kwa wahusika watu wazima ambao washatamauka na maisha. Tunaona kwamba utajiri hauji bure ila kwa kuhangaika na kazi. Kazikwisha na Bimkubwa wote walikua wakulima. Ina maana kwamba ukulima ndio nguzo kuu katika maisha.

Aartsen, M., & Jylha, M., (2011). Onset of loneliness in older adults: results of a 28-year prospective study. *European Journal of Ageing,* 8, 31-38.

Abrams, M. H. A. (1981). *Glossary of Literary Terms*. Holt, Rinehart and Winston.

Alfaro, M. J. M. (1996). 'Intertextuality: Origins and Development of the Concept'. *Atlantis XVIII* (1-2), 268- 285.

Arege, T. M. (2009). *Kijiba cha Moyo*. Sasa Sema.

Arege, T. M. (2009). *Mstahiki Meya*. Vide-Mulwa Publications.

Bakhtin,R (1981). *The Dialogic Imagination: Four Essays*. University of Texas Press

Barthes, R. (2007). 'From Work to Text'. Katika B. Das, & J. M. Mahanty (Wah.). *Literary Criticism: A Reading*. Oxford UniversityPress, 413420.

Bosire, T. B. (2016). *Mwingilianomatini kati ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali na Mstahiki Meya.* (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Bosma, H., Jansen, M., Schefman, S., Hajema, K., & Feron, F., (2015). Lonely at the bottom: A crosssectional study on being ill, poor, and lonely. *Public Health,* 129,185-87.

Cacioppo, J.T., Hawkley, L.C., & Thisted, R.A., (2010). Perceived Social Isolation Makes Me Sad: 5Year Cross-Lagged Analyses of Loneliness and Depressive Symptomatology in the Chicago Health, Aging, and Social Relations Study. *Psychology and Aging,* 25, 453-63.

De Saussure, F. (2006). *Writings in General Linguistics* (trans. C. Sanders & M. Pires). Oxford University Press.

Euphrase, K. (1971). *Rosa Mistika*. East African Publishers.

Fokkema, T., Gierveld, J.D.J., & Dykstra, P.A.(2012). Cross-National Differences in Older Adult Loneliness. *Journal of Psychology,* 146, 201-28.

Gogol, N. (1836). *The Government Inspector*. Oxford University.

Goodenow, C., Watson, R. J., Adjei, J., Homma, Y., & Saewyc, E. (2016). Sexual orientation trends and disparities in school bullying and violence-related experiences, *1999–2013*. *Psychology of Sexual Orientation and Gender Diversity*, 3(4), 386–396.

Haberer, A. (2007). "Intertextuality in Theory and Practice". *Literatura*, 49/5, 54-67.

Hansen, T., & Slagsvold, B. (2015). Late-Life Loneliness in 11 European Countries: Results from the Generations and Gender Survey. *Social Indicators Research*, 124 (1), 1-20.

Hsieh, N., & Liu, H. (2021). Social relationships and loneliness in late adulthood: Disparities by sexual orientation. *Journal of Marriage and Family*, 83(1), 57–74.

Hussein E. (1971). *Mashetani*. Oxford University Press.

Juan, R. (1955). *Pedro Paramo*. Fonde de Cultura Economica

Kenya Literature Bureau. (2016). *Kamusi Pevu ya Kiswahili*. Vide Muwa Publishers.

Kiimbila, J. (1966). *Lila na Fila*. Longmans.

Kirumbi, S. (1974). *Nataka Iwe Siri*. TUKI.

Kristeva. J. (1977). *Word, Dialogue, and Novel. Desire in Language: A Semiotic Approach to Literature and Art*. Columbia University Press.

Kristeva, J. (1980). *Desire in Language: A Semiotic Approach to Literature and Art*. Blackwell.

Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili*. Mture Education Publisher.

Matundura, E. (2008). *Sitaki Iwe Siri*. Longhorn Publishers.

Mazrui, A. (1981). *Kilio cha Haki*. Longhorn Publishers

Mbogo, E. (1980). *Giza Limeingia*. Tanzania House

Mohamed, S. A. (1990). *Tata za Asumini*. Longman.

Mohammed, S. A. (1995). *Amezidi*. East African Educational Publishers.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya uhakiki wa Fasihi*. East African Educational Publishers Ltd.

Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. TUKI.

Mwachofi, A. (1987). *Mama ee*. East Africa Publishers.

Ndalu, A., & Babusa, H. (2013). *Kamusi Teule ya Kiswahili Kilele cha Lugha*. East African

Njogu, H. G. (2007). Mwingilianomatini katika fasihi ya Kiswahili: Tata za Asumini na Rosa Mistika. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Njogu, K., & Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K., & Chimera, R. (2011). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K., & Wafula, M. R. (2013). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Jomo Kenyatta Foundation

Njoroge, H. (2007). *Mwingilianomatini katika Fasihi ya Kiswahili: Tata za Asumini na Rosa Mistika*. (Tasnifu ya MA). University of Nairobi.

Perales, F., & Campbell, A. (2020). Health disparities between sexual minority and different-sex-attracted adolescents: Quantifying the intervening role of social support and school belonging. *health*, 7(3), 146–154.

Shaaban,R. (1951). *Kusadikika. Nchi Iliyo Angani*. Nelson

Shaaban, R. (1952). *Adili na Nguguze*. Macmillan.

Shaaban, R. (1966). *Utubora Mkulima*. Mkuki na Nyota Publishers.

Shitakwa, A (2018*) Mwingilianomatini Katika Riwaya Ya Utengano Na Safari Ya Lamu*. (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Moi.

Syambo, B., & Mazrui, A. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi*. East African Educational Publishers.

TUKI. (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Oxford University Press.

Waititu, F., & Ipara, I. (2018). *Ijaribu na Uikarabati*. Oxford University Press

Walibora, K. (1996). *Siku Njema*. Longhorn Publishers.

Wamitila, K. W. (2003a). 'Influence or Intertextuality? A comparative Study of Kezilahabi's Nagona and Mzingile and Juan Rulfo's Pedro Paroma'. *KISWAHILI*, 66, 49-58.

Wamitila, K. W. (2003b). *Kamusi ya Fasihi*: *Istilahi na Nadharia*. Focus Books.

Wamitila, K.W. (2008). *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Vide Muwa Publishers.

Wanyela. S. (2007). *Matumizi ya ushairi katika tamthilia ya Kiswahili*. (Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo kikuu cha Kenyatta.

Watt, I. (1957). *The Rise of the Novel: Studies in Defoe, Richardson and Fielding*. University of California Press.